**JAMUHRI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI**

CHIDYA SEKONDARI
S.L.P. 324

MASASI - MTWARA,

ChidyaSec@gmailcom,

**Namba za simu**

Mkuu wa Shule : 0784483628
Makamu Mkuu wa Shule: 0712921704
Mwalimu wa Taaluma: 0655398198

MZAZI/MLEZI WA ……**.....**

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2022**

Nafurahi kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii.Hongera sana.Soma kwa makini maelezo na maagizo yote yaliyomo kwenye kila kipengele cha barua hii na kuyatekeleza. Shule ya sekondari chidya iko wilaya ya masasi, mkoa wa mtwara. Kutoka masasi stendi ya mabasi hadi chidya sekondari ni km 33. Kuna basi ambalo hufanya safari kati ya masasi na chidya kila siku. Gari hilo huondoka masasi saa 6:30 -7:00mchana. Watakaosafiri kwa gari binafsi wanaweza kufika chidya kwa kuanzia chigugu au namakongwa ambavyo ni vijiji. Naulli kwa gari kutoka masasi hadi chidya kwa sasa ni Tshs 3000/=.

**KUFUNGUA SHULE:**

Shule itafunguliwa tarehe 09/01/2022 kwa muhula wa kwanza wa masomo. Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni si zaidi ya tarehe 02/01/2022.

**2:1 SARE ZA SHULE**

1. Mwanafunzi aje na suruali mbili za rangi ya kaki chini ziwe **inch 7 (ISISHONWE KWA MFUMO WA MODO WALA ISIBANE).**
2. Mashati mawili meupe yenye mikono mifupi ( aina ya tomato)

3. Jozi mbili za viatu vya ngozi rangi nyeusi
4. Jozi mbili za soksi rangi nyeusi
5. Sweta moja rangi ya kijani (lisiwe na maandishi yoyote) kwa ajili ya wakati wa baridi
6. Aje na tai nyeusi (ndefu) saizi ya kati
7. Mkanda mweusi wa ngozi

**2:2 SARE ZA MICHEZO**

1. Track suit za rangi ya blue bahari.
2. Raba jozi moja.

**2:3 SARE ZA KUSHINDIA**

1. Aje na suruali mbili za rangi nyeusi (za kitambaa na zishonwe kama namba 2:1:1 ilivyoelekeza)

2. Aje na T-shirt mbili za rangi ya njano zenye kora ( zisiwe na maandishi yoyote)

**3:1 MAHITAJI MENGINEYO**

01. kivuli cha cheti cha kuzaliwa (BIRTH CERTIFICATE)
02. madaftari (counter book) dazeni moja ,kalamu za wino, penseli, rula na mathematical set( vinapatikana kwenye duka la shule)
03. Mwanafunzi aje na gogoro la sponji upana wa ft 2.5 au atapata shuleni kwa Tsh 35000/=
04. Blanketi 01
05. Shuka 02 za rangi ya kijani
06. Taulo 01
07. Chandarua rangi ya blue ya pembe nne
08. Mto mmoja
09. Kandambili jozi 01
10. Vyombo vya chakula; sahani, bakuli,kikombe,kijiko,dumu la lita 03 au 05 kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kunywa.
11. Madaftari madogo 4 kwa ajili ya mazoezi
12. Graph pad 02(mdaftari ya graph paper)
13. Rimu moja ya karatasi.
14. Kiti kimoja cha plastiki rangi ya blue.

## 3:2 VIFAA VYA KAZI NA USAFI

1. Jembe na mpini wake
2. Mopa au zinapatikana shule kwa tsh 5,000/=
3. Ndoo mbili ya ujazo wa lita 10.
4. Fagio ngumu za plastiki za chooni.
5. Sabuni ya maji ya chooni lita 5 inapatikana shuleni kwa tshs.7,500/=
6. Fagio raini (soft bloom) na chelewa

## 3.3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha , inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni - preparation
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
i) Kutunza mali za umma.
j) Kutii mabadiliko yoyote yatakayoathiri mabadiliko ya ratiba ya shule.
k) Marufuku kucheza lizangati eneo la shule

## 3.4. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

a) Wizi
b) Usherati na ushoga

c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine , mirungi, kubeli na kadhalika. e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali za umma
g) Kudharau Bendera ya Taifa.
h) Uvutaji wa sigara
i) Kufuga ndevu
j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
k) Kukataa adhabu kwa makusudi
l) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
m) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa
n) Kutoa lugha chafu kwa walimu , wanafunzi wenzake, walezi na jamii kwa ujumla.
o) Kushiriki matendo ya uharifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
p) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
q) Kutembelea majumba ya starehe au nyumba za kulala wageni.
r) Kufanya jaribio lolote au kutishia kujiua kama kunywa sumu.

**N.B:** *WAZAZI / WALEZI HAKIKISHENI WATOTO WENU WANAPIMA AFYA NA KUTOA TAARIFA ZA UKWELI SHULENI.MAELEKEZO YATAKAYOELEZWA NA MWANAFUNZI BILA KUWEPO NA UTHIBITISHO WA DAKTARI HAYATASIKILIZWA*

KARIBUNI SANA CHIDYA SEKONDARI

MKUU WA SHULE
CHIDYA SEKONDARI
S.L.P.324 MASASI

**ZAWADI S. MDIMBE MKUU WA SHULE.**

**PRESIDENT,S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

Chidya secondary school
P.o.Box 324
MASASI
……..

.
The Medical Officer
……
……..
……

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

NAME OF STUDENT……

Please examine the above named student to his fitness as indicated below.This certificate must be signed by a qualified Medical Officer of a Government hospital or Health centre.

1. Stool……
2. Urine……
3. Veneral Diseases……..
4. T.B……
5. Eye……...
6. Ear……
7. Chest……..
8. Abdomen……..
9. Skin……...
10. Any other physical disability……..

I certify that the above student is fit/not fit to pursue secondary education as indicated above.

NAME OF MEDICAL OFFICER……
SIGNATURE OF MEDICAL OFFICER……..
DESIGNATION……..
STATION……..OFFICIAL STAMP……
DATE.....

**KUMBUKUMBU MUHIMU ZA MWANAFUNZI**

**(IJAZWE KABLA YA KURIPOTI SHULENI)**

A.1.JINA LA MWANAFUNZI……..

2.(a)Jina la baba/mlezi ……Passportsize

(b)Kazi ya baba,mlezi……

(c)Mahali anakoishi.

Kijiji/Mtaa……..Kata……

Wilaya/Mji……Mkoa……

Namba ya simu……..Email……

3.(a)Jina la mama/mlezi……Passportsize.

(b)Kazi ya mama,mlezi……

(c)Mahali anakoishi.

Kijiji/Mtaa……..Kata……

Wilaya/Mji……Mkoa……

Namba ya simu……..Email……

**B.NDUGU WA KARIBU.**

| NA. | JINA | UHUSIANO | MAHALI NAPOISHI | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| **01** | | | | |
| **02** | | | | |
| **03** | | | | |
| **04** | | | | |

NB:Njoo na picha za ndugu wote wa karibu

## C.MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO/FUJO NA MAKOSA YA JINAI.

Mimi…….(mwanafunzi),naahidi kuwa sitajihusisha/sitashiriki katika kupanga,kufanya wala kushabikia migomo,fujo au ghasia zozote au  makossa ya jinai nikiwa Chidya sekondari katika muda wangu wa uanafunzi.

Sahihi……..tarehe…….